JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

UANDAAJI MPANGO SHIRIKISHI JAMII KWA MFUMO WA FURSA NA VIKWAZO KWA MAENDELEO

KIONGOZI CHA MCHAKATO WA KIJIJINI

S.L.P 1923
DODOMA

Novemba, 2007

YALIYOMO

MAANDALIZI YA MCHAKATO WA KIJIJINI 1
HATUA ZA AWALI 1
ZIARA YA MAANDALIZI 1
RATIBA YA KILA SIKU YA MCHAKATO KIJIJINI 4
SIKU YA KWANZA: Maandalizi ya Jamii na Kukusanya Takwimu 4
SIKU YA PILI: Maandalizi ya Jamii na Ukusanyaji wa Takwimu 4
SIKU YA TATU: Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji 5
Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji 5
Kuchora Ramani ya Kijiji 6
Tathmini ya Uwezo wa Kujikimu wa Kaya 7
SIKU YA NNE: Kukusanya Takwimu kwa kutumia Zana Shirikishi 9
Matembezi Mkato (Kataa ya njia) 10
Matukio ya Kihistoria 11
Kalenda ya Msimu 12
Uchambuzi wa Taasisi 14
Uchambuzi wa Shughuli za Kiuchumi na Kijamii katika Mazingira 17
Ramani ya Umilikaji Rasilimali Kijinsia 19
Shughuli za Kutwa Kijinsia 21
Vyanzo vya Mapato na Matumizi 23
SIKU YA TANO: Kujadili Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 24
SIKU YA SITA: Kujadili Dira ya Taifa ya Maendeleo 28
SIKU YA SABA: Kujadili Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 33
SIKU YA NANE: Kuandaa Rasimu ya Mpango 35
SIKU YA TISA: Mkutano wa Halmashauri ya Kijiji 37
Kuweka Vipaumbele 38
Kuandaa Rasimu ya Mpango wa Miaka Mitatu 39
SIKU YA KUMI: Mkutano Maalum wa Kamati ya Maendeleo ya Kata 39
SIKU YA KUMI NA MOJA: Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji 40
SIKU YA KUMI NA MBILI: Muhtasari wa Shughuli za Utekelezaji 40
KIAMBATISHO I: FOMU YA TAKWIMU 42
KIAMBATISHO II: RATIBA YA MCHAKATO WA KIJIJINI 47

MAANDALIZI YA MCHAKATO WA KIJIJINI

HATUA ZA AWALI

Kufahamisha uongozi wa Kijiji juu ya kuwepo kwa zoezi la kuandaa Mpango Shirikishi Jamii wa Kijiji. Tuma barua ya taarifa. Katika barua hiyo, taja siku mtakayofanya ziara ya maandalizi ya awali. Wafahamishe waandae takwimu muhimu za Kijiji kwa ajili ya kuandaa mpango. Barua hiyo iujulishe uongozi wa Kijiji kuitisha Kikao Maalum kitakachojumuisha viongozi wa Kijiji na watu mashuhuri wakati wa ziara ya maandalizi. Aidha barua itaje waziwazi watu wote muhimu watakaoalikwa katika kikao hicho.

ZIARA YA MAANDALIZI

Kabla ya kuanza Mchakato wa kuandaa Mpango Shirikishi Jamii wa Kijiji, kwa kushirikisha Jamii ifanyike ziara ya maandalizi kukutana na viongozi wa Halmashauri ya Kijiji, watumishi wa ugani waliopo katika Kijiji na baadhi ya watu mashuhuri. Wakati wa ziara hiyo, Wawezeshaji, watafafanua kwa usahihi Malengo ya Dira ya Taifa ya maendeleo 2025. Jamii ikielewa vizuri Malengo ya Dira ambayo ndiyo mwongozo wa kisera, itaweza kupanga mpango wake wa maendeleo kwa ufanisi. Kutokana na malengo makuu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo, watawezeshwa kuweka vipaumbele kulingana na hali halisi ya Kijiji.

Shughili nyingine muhimu wakati wa maandalizi ya Jamii, ni kufanya majadiliano kati ya Wawezeshaji na uongozi wa Kijiji kuhusu njia zinazofaa kutumika wakati wa uhamsishaji kabla ya Mkutano Mkuu wa Uzinduzi wa Mchakato. Njia mbalimbali zinaweza kutumika kuhamasisha Jamii kulingana na mazingira yaliyopo. Katika baadhi ya Jamii vikundi vya uhamasishaji vilivyopo kama vile vya vijana na vya ngoma vinaweza kutumika. Katika Jamii nyingine, njia kama kutembelea nyumba kwa nyumba, kupeana habari katika mikusanyiko mbalimbali na matangazo kupitia vipaza sauti vinaweza kutumika. Majadiliano katika mkutano huo yatahusu yafuatayo:

- Watakaoshiriki katika Mchakato wa Mpango Shirikishi.
- Uhamasishaji wa Jamii.
- Ratiba ya Mchakato.
- Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na kuchagua malengo yatakayotumika kuandaa mpango.
- Kukusanya takwimu muhimu za Kijiji.
- Kuandaa orodha ya Wakuu wa Kaya kwa kila Kitongoji. Orodha hii ibainishe kaya zinazoongozwa na wanaume na wanawake, walemavu, vikongwe na wajane kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo (angali jedwali 1)

Jedwali 1: Orodha ya Wakuu wa Kaya

Kijiji……. Kitongoji…….

Na	Jina la mkuu wa kaya	Jina maarufu	Jinsi		Watotowalio Katika Mazingira magumu	Mjane	Kikongwe	Mlemavu	Waweka alama				Alama	Hali
			Ke	Me					1	2	3	4		

- Eleza kwamba katika zoezi hili yataundwa makundi mahususi kwa ajili ya majadiliano, na kuwa utaratibu wa makundi hayo, utazingatia uwakilishi ulio sawa kwa kila Kitongoji, jinsi na rika.
- Uongozi wa Kijiji utoe taarifa na kuhamasisha wakazi wote(wananwake, wanaume na vijana) waweze kuhudhuria mkutano wa Uzinduzi wa Mchakato bila kukosa.

RATIBA YA KILA SIKU YA MCHAKATO KIJIJINI

SIKU YA KWANZA: Maandalizi ya Jamii na Kukusanya Takwimu

Shughuli kuu: Maandalizi ya Jamii na kukusanya takwimu muhimu za Kijiji

Siku ya kwanza ni ya maandalizi ya Jamii na ukusanyaji wa takwimu muhimu za Kijiji.

Wawezeshaji, Halmashauri ya Kijiji, na vikundi vya uhamasishaji, wataendelea kuhamasisha Jamii juu ya kushiriki katika Mchakato. Mwezeshaji ataviwezesha vikundi vya Jamii ambavyo vitasambaza taarifa Kijijini. Pamoja na hayo mambo yafuatayo yataendelea kusisitizwa:

- Umuhimu wa Mpango Shirikishi Jamii
- Ushiriki wa Jamii katika Mkutano Mkuu wa Uzinduzi wa Mchakato

Ni vema kuwezesha vikundi hivyo kwa umakini zaidi ili ujumbe ueleweke kwa urahisi na kufikishwa vizuri katika Jamii. Endapo kuna uwezekano, uwezeshaji na uhamasishaji unaweza kuanza siku hiyo (ya kwanza) na kisha siku ya pili kuendelea kusambaza taarifa kwa Jamii kwa kutumia mbinu mbalimbali zilizotajwa hapo awali. Vikundi ya uhamashaji vitafikisha ujumbe kwa Jamii kwa kushirikiana na viongozi wa Jamii wakiwa ni waratibu pamoja na Wawezeshaji.

SIKU YA PILI: Maandalizi ya Jamii na Ukusanyaji wa Takwimu

Shughuli kuu: Maandalizi ya Jamii na kukusanya takwimu muhimu za Kijiji

Maandalizi ya Jamii yanaendelea kufanyika na takwimu zinaendelea kukusanywa.

SIKU YA TATU: Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji

Shughuli kuu: Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji wa Uzinduzi wa Mchakato

Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji wa uzinduzi utafanyika siku ya tatu ya Mchakato. Shughuli zitakazofanyika siku hiyo ni;

- Wawezeshaji kukusanya fomu za orodha ya Wakuu wa Kaya.
- Kuthibitisha Malengo ya Dira ya Taifa ya maendeleo ya 2025 yaliyochaguliwa katika Mkutano wa Halmashauri ya Kijiji.
- Kuchagua Wawezeshaji wa Jamii 6 -10 .
- Kuchagua makundi mahususi kwa kuzingatia uwakilishi wa vitongoji, jinsi na rika
- Kuchora Ramani ya Kijiji.
- Kuweka vigezo vya uwezo wa kujikimu katika kaya
- Kufanya tathmini ya uwezo wa kujikimu wa kaya
- Afisa Mtendaji wa Kijiji kuendelea kukusanya takwimu (takwimu za upili)

Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji

Yafuatayo ni mambo muhimu ya kuzingatia:-

- Mwenyekiti wa Kijiji atafungua mkutano.
- Mkutano utahudhuriwa na wanaKijiji wote wenye stahili.
- Mwenyekiti awape nafasi Wawezeshaji ili wajitambulishe. Kisha awatambulishe viongozi, wageni mbalimbali, watumishi wa ugani na wadau wengine wa maendeleo waliopo Kijijini.
- Mwenyekiti aeleze lengo na madhumuni ya mkutano. Hii inaweza kufanyika kwa kusoma barua ya utambulisho iliyoandikwa kutoka Halmashauri ya Wilaya.
- Mwenyekiti wa Kijiji awasilishe Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 yaliyojadiliwa na wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji ili kutoa fursa kwa Jamii kuelewa, na hatimaye kuandaa Mpango kwa kuzingatia mwongozo wa Dira.
- Afisa Mtendaji wa Kijiji atawasilisha ratiba ya Mchakato ipitiwe na kuthibitishwa.

Kuchora Ramani ya Kijiji

Ramani ya Kijiji itaonesha mipaka, rasilimali za kiasili na zilizotengenezwa na binadamu (barabara, mito, ziwa, misitu, mabonde, milima, umeme, visima, vituo vya maji), Taasisi (shule, zahanati, kanisa, msikiti). Ramani ya Kijiji itachorwa na kundi la watu 6 -10 waliochaguliwa katika Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji.

Mfano wa Ramani ya Kijiji: Ramani ya Kijiji cha Nrao Kisangara – Wilaya ya Hai



Hatua za kufuata wakati wa kuchora ramani:-

1. Waelekeze wanakikundi wa ramani wachague mahali/ eneo panapofaa kuchorwa Ramani ya Kijiji kwenye sehemu ya ardhi iliyo tambarare.
2. Waelekeze kuwa ramani itachorwa na wao kwa kutumia rasilimali zilizopo kama vile mawe, vijiti, majani, majivu.
3. Waelekeze waelekee jua linapotokea na kuzama ili iwe rahisi kubaini kaskazini.

4. Ramani ioneshe vitu vyote muhimu ikiwemo mipaka ya vijiji jirani, mipaka ya vitongoji, Taasisi zilizopo, rasilimali zilizopo na miundo mbinu muhimu.
5. Katika uchoraji wa ramani wageni wasichukue hatamu, bali washauri na kukumbusha tu.
6. Wageni watoe ushauri juu ya ushiriki wa jinsi ya kuendelea na zoezi, kwa mfano, kushauri ramani itakapokubalika ihamishiwe katika karatasi na mwanaKijiji atakayejitolea au kuchaguliliwa.
7. Baada ya kuchora ramani, washukuruni wananchi na kuwakumbusha kwamba zoezi litaendelea siku ya pili.

Tathmini ya Uwezo wa Kujikimu wa Kaya

Tathmini ya uwezo wa kujikimu wa kaya ni Zana Shirikishi inayochambua uwezo wa kiuchumi wa kila kaya. Vigezo vitakavyotumika ni vile vilivyowekwa na Mkutano Mkuu Maalum.

Hatua za kufuata katika tathmini ya uwezo:

1. Kila Mwenyekiti wa Kitongoji atakuwa na orodha ya Wakuu wa Kaya atakayoikabidhi kwa mwezeshaji.
2. Kila Mwenyekiti wa Kitongoji atawezeshwa kuchagua wawakilishi wanne kwa kuzingatia jinsi (me:2 na ke:2) kwa ajili ya kuweka alama. Wawe wanawafahamu vizuri wakazi wa Kitongoji.
3. Baada ya Mkutano Mkuu, waweka alama waliochaguliwa, watakaa kivitongoji.
4. Mwezeshaji aeleze jinsi ya kuendesha zoezi.
5. Orodha ya Wakuu wa Kaya kwa kila Kitongoji itatumika kuainisha uwezo wa kaya wa kujikimu.
6. Wawakilishi wanne kutoka kila Kitongoji wataweka alama zifuatazo kwa kila kaya:
    - Hali duni 1- 2
    - Hali nafuu 3
    - Hali nzuri 4 -5
7. Jumla ya alama zilizopatikana kwa kila mkuu wa kaya zitatoa tafsiri ifuatayo:
    - Duni: 4 - 8
    - Nafuu: 9 - 15
    - Nzuri: 16 - 20

Jedwali 2 Tathmini ya uwezo wa kujikimu wa kaya: Kijiji cha Nrao kisangara

Na.	Jina la mkuu wa kaya	Waweka alama				Jumla	Hali ya uwezo
		1	2	3	4		
1	Iddi	1	2	1	2	6	Duni
2	Ramadhani	5	4	5	4	18	Nzuri
3	Doto	3	2	4	3	12	Nafuu

Matokeo ya kila Kitongoji hukusanywa na kujumlishwa na hivyo kuwezesha kupatikana matokeo yote ya Kijiji ambapo asilimia na idadi ya kaya kiuwezo hupatikana

Jedwali 3 Tathmini ya jumla ya uwezo wa kujikimu wa kaya: Kijiji cha Nrao Kisangara

Kitongoji	Duni	Nafuu	Nzuri	Jumla ya kaya
Kisangara	30	10	5	45
Nrao juu	52	27	13	92
Ifunu	67	22	10	99
Nrao chini	43	17	9	69
Jumla	192	76	37	305
Asilimia	63%	25%	12%	100%

jedwali 4 Tathmini ya jumla ya uwezo kwa kuzingatia kaya zenye hali duni

Kitongoji	Idadi ya kaya	Mkuu wa kaya				
		Me	Ke	Majane	Kikongwe	Mtoto aliye katika mazingira magumu
Kisangara	30	13	6	4	4	3
Nrao juu	52	20	16	6	6	4
Ifunu	67	50	8	4	3	2
Nrao chini	43	23	8	5	5	2
Total	192	106	38	19	18	11
Percent	100%	55%	20%	10%	9%	6%

SIKU YA NNE: Kukusanya Takwimu kwa kutumia Zana Shirikishi

Shughuli kuu: kukusanya takwimu kwa kutumia Zana Shirikishi Jamii

Wawezeshaji wawaelekeze viongozi wa Kijiji kuwa shughuli kuu zitakazofanyika siku hiyo ni kukusanya takwimu kwa kutumia Zana Shirikishi zifuatazo:-

- Ramani ya Umilikaji Rasilimali Kijinsia
- Uchambuzi wa vyanzo vya Mapato na Matumizi
- Matembezi Mkato (Kataa ya njia)
- Uchambuzi wa Taasisi
- Kalenda ya Msimu
- Historia ya Matukio Muhimu
- Shughuli za Kutwa Kijinsia

Matembezi Mkato (Kataa ya njia)

Matembezi Mkato yafanyike asubuhi yakiongozwa na Wawezeshaji wa Kijiji walioshiriki katika kuchora ramani. Zoezi la Matembezi Mkato likishakamilika washiriki (Wawezeshaji na wananchi walioshiriki) wakutane kuandaa na kukubaliana yaliyojitokeza kwenye Kataa ya njia na kisha kuweka kielelezo.

Kataa ya njia – Kijiji cha Nrao Kisangara Wilaya ya Hai



	Bondela Iima	Kisangara	Bondela Okyoro	Nrao Juu	Kyungukyena
Udongo	Udongo mweusi na mwekundu kidogo	Mwekundu	Mwekundu	Udongo mwekundu	Udongo wa usena
Uoto	Miti ya asili kutotesha migomba, kahawa, majani	Miti ya asili, kuotesha mibuni, migomba na majani ya mifugo	Miti ya asili na kuotesha migomba na mibuni	Miti ya matunda, miti ya asili ya kuotesha mibuni, migomba, majani ya mifugo	Miti ya sili, migomba na mibuni kidogo na majani
Shughuli	Kilimo cha mboga, mahindi, miwa, viazi, majimbi n.k.	Kilimo cha mibuni na migomba	Kilimo cha mibuni na migomba	Kilimo cha mibuni, migomba na mboga	Kilimo cha mibuni na migomba kidogo
Makazi	Hakuna	Yapo	Hakuna	Yapo mengi	Hakuna
Huduma	Hakuna	Kanisa, shule, bonde la maji, mfereji, duka, barabara	Hakuna	Shule, ofisi ya kijiji, umeme, bomba la maji, mfereji, mashine ya kusaga, chama cha ushirika, duka na barabara	Mfereji
Fursa	Miti ya mbao matunda, mfereji, mto na ardhi	Miti ya mbao matunda, ardhi, nguvu kazi	Miti ya mbao, matunda, ardhi kidogo	Ardhi kidogo yenye rutuba, miti ya mbao, nguvu kazi kubwa, majani ya mifugo	Miti ya mbao na majani ya mifugo
Vikwazo	Eneo dogo la ardhi,	Ongezeko la wakaazi/ ongezeko la watu	Mteremko mkali	Ongezeko la makaazi/ msongamano wa watu	Mmomonyoko wa ardhi na mteremko mkali

Matukio ya Kihistoria

Matukio ya kihistoria ni Zana Shirikishi inayowezesha Jamii kuchambua mlolongo wa matukio muhimu ambayo yalitokea. Jamii huainisha matukio makubwa ya kihistoria yaliyotokea, sababisho, athari au manufaa yaliyotokana na matukio hayo. Hatua zilizochukuliwa kurekebisha hali hiyo kama ilikuwa mbaya. Aidha zana hii huwezesha Jamii kujifunza namna ya kukabiliana na maafa/ janga/ tukio na kuiga mikakati inayofaa. Zifuatazo hapa chini ni hatua za kufanya zoezi la matukio ya kihistoria.

Hatua

1. Mwezeshaji aanzishe mazungumzo kwenye kikundi mahsusi kwa kuwauliza matukio muhimu wanayoyakumbuka kutokea ndani ya Kijiji chao. Hapa ni matukio yote mazuri na mabaya.
2. Wawezeshe wayataje kwa kufuata miongo na kama watashindwa basi wataje kwa kadiri wanavyokumbuka.
3. Wawezeshe waeleze faida/ hasara waliyoipata kutokana na tukio hilo.
4. Waeleze walichukua hatua gani kutatua au kukabiliana na tukio hilo.
5. Kama ni tukio zuri, waombe waeleze mafanikio yaliyopatikana na nini?
6. Andaa jedwali la historia ya Kijiji.

Mfano wa Matukio ya Kihistoria katika Kijiji cha Nrao Kisangara.

Mwaka	Tukio	Sababisho	Madhara/ Manufaa	Ufumbuzi/ Matokeo
1939	Njaa	Nzige waliharibu mazao	• Upungufu mkubwa wa chakula • Mifugo ilikufa.	• Mifugo iliuzwa, ili kunua chakula. • Kutumia kilimo cha umwagiliaji na kupanda mazao yanayokomaa mapema kama vile viazi na mbogamboga.
1940	Barabara ya lami kufika Kijijini	Kusafirisha nafaka kutoka mashamba makubwa ya Kilimanjaro magharibi.	• Usafiri rahisi na wa uhakika. • Kuongezeka kwa uzalishaji na kuanzishwa kwa masoko mapya	

Kalenda ya Msimu

Kalenda ya Msimu ni Zana Shirikishi inayotumika kuwezesha kutambua shughuli mbalimbali zinazofanyika katika Jamii katika kipindi maalum. Kwa kawaida Kalenda huanzia Januari na kuishia Desemba. Lakini kwa maeneo ya vijijini kalenda huanzia wakati wa msimu wa mvua ambapo hutofautiana kati ya eneo na eneo. Mwanzo wa msimu hutofautiana toka sehemu hadi sehemu kufuatana na shughuli zinazofanyika na wahusika.

Hatua

Ukiwa bado na kundi mahususi waombe waelezee hali za msimu zilivyo pale Kijijini, kwa kutaja:

1. Lini au miezi gani mvua huwa zinanyesha
2. Ni miezi gani huwa ni ya kiangazi
3. Waeleze ni mazao gani yanayolimwa Kijijini kwa ajili ya chakula na biashara.
4. Wajadiliane pia shughuli mbalimbali zinazofanywa Kijijini kama vile, ujenzi wa nyumba, kucheza ngoma.
5. Waombe waeleze matatizo ya milipuko ya magonjwa na hutokea lini?
6. Kwa shughuli namba tatu na nne ionyeshwe kwa kawaida hufanywa na nani kijinsia.

Jedwali 6: Mfano wa Kalenda ya Msimu

	Kalenda ya msimu- Kijiji cha Nrao kisangara											
Maelezo	**J**	**F**	**M**	**A**	**M**	**J**	**J**	**A**	**S**	**O**	**N**	**D**
1. Hali ya hewa												
Mvua												
2.Shughuli za kilimo												
Kilimo cha mahindi												
Kulima												
kupanda												
kupalilia												
Kuweka mblea												
Kuvuna												
3. kilimo cha ndizi/kahawa												
kupalilia												
Kukata matawi												
Kupuliza dawa												
Kuvuna												
4. magonjwa ya binadamu												
Malaria												
Vichomi												
kuharisha												
5. Kilimo cha matunda na mbogamboga												
Nyanya												
Parachichi												
Mchicha												
Kabeji												
6. Shughuli za Utawala												
Nguvukazi												
Upatikanaji wa chakula												

Uchambuzi wa Taasisi

Uchambuzi wa Taasisi unahusisha kuangalia aina tatu za mahusiano;

- Mahusiano kati ya Taasisi na Jamii
- Mahusiano kati ya Taasisi za ndani ya Jamii
- Mahusiano kati ya Taasisi za nje na Jamii

Mahusiano kati ya Taasisi za ndani na Jamii

Hatua

1. Wezesha kundi mahususi kutaja Taasisi zote za nje na ndani.
2. Ziorodheshe na zipange kulingana na umuhimu wake katika Jamii.
3. Wezesha kundi mahususi kukata kadi za ukubwa tofauti na waandike majina ya Taasisi kulingana na umuhimu wake. Kadi kubwa inawakilisha Taasisi yenye umuhimu mkubwa zaidi kwa Jamii na kadi ndogo ni kinyume chake.
4. Chora mduara mkubwa unaowakilisha Jamii. Mduara unaweza kuchorwa juu ya ardhi au kwenye bango kitita kulingana na ukubwa wa kundi mahususi.
5. wezesha kundi mahususi kubandika kadi katika mduara kulingana na umuhimu wake. Kadi zitakazobandikwa karibu na kitovu cha Jamii zinawakilisha Taasisi zenye mahusiano mazuri na Jamii. Zilizobandikwa mbali na kitovu maana yake hazina mahusiano mazuri na Jamii. Kwa maana nyingine, jinsi kadi ya Taasisi ilivyowekwa mbali na kitovu cha mduara ndivyo mahusiano yanavyozidi kupungua.
6. Mshiriki mwingine anaweza kuhamisha kadi kwa kadiri anavyoona inafaa na kuiweka sehemu nyingine. Mshiriki atoe sababu za kuhamisha kadi hiyo kwa kuzingatia huduma inayotolewa na Taasisi na majadiliano yafanyike hadi watakapofikia muafaka.

Kielelezo 1: Mahusiano baina ya Jamii na Taasisi



Matokeo ya uchambuzi wa Taasisi za ndani yaingizwe katika jedwali kama inavyooneshwa hapa chini:

Jedwali 7: Taasisi na umuhimu wake

Taasisi	Shughuli	Umuhimu	Nafasi ya kimahusiano	Maoni
Halmashauri ya Kijiji	utawala	1	4	– Mikutano ya Kijiji haiitishwi – Hakuna uwazi katika Mapato na Matumizi.
Msikiti	Elimu na Ibada	2	1	– Kutoa ushauri – Wamejenga shule ya awali tu
Shule	Elimu	3	2	– Matokeo mazuri ya mitihani
Kanisa	Huduma za kiroho	4	3	– Wanatoa mafundisho ya maadili mema

Mahusiano kati ya Taasisi na Taasisi

Hii ni zana inayoiwezesha Jamii kuchambua mahusiano kati ya Taasisi na Taasisi

1. Kwa kutumia kadi kama ilivyotumika katika kielelezo 1 jadili mahusiano yaliyopo kati ya Taasisi na Taasisi.
2. Jamii wajadili na kupanga katika mduara (chapati) kuonyesha Taasisi zinazohusiana (kushirikiana) katika kutoa huduma kwa Jamii.
3. Jamii waeleze jinsi uhusiano wa Taasisi hizo unavyokuza huduma za Jamii.
4. Jamii pia waeleze Taasisi zinazotoa huduma zinazofanana na mahusiano yao.

Kielelezo 2: Mahusiano kati ya Taasisi na Taasisi



Kadi ambazo zinazoungana zinaonesha Taasisi zenye mahusiano mazuri katika kutoa huduma.

Mahusiano ya Jamii na Taasisi zilizo nje ya Kijiji

Tumia mchoro wa chapati kuonyesha mahusiano yaliyopo baina ya Jamii na Taasisi zilizopo nje ya Kijiji. Jinsi mshale wa Taasisi unavyokuwa jirani na kitovu cha Kijiji, ndivyo Taasisi hiyo ilivyo muhimu kwa Jamii.

Kielelezo 3: Mahusiano ya Taasisi za nje na Jamii



Taasisi za nje zenye mishale iliyo karibu na kitovu zina mahusiano ya karibu na Jamii na zile ambazo mishale inakomea mbali ni kinyume chake. Ukubwa wa chapati unaonesha umuhimu katika Jamii.

Uchambuzi wa Shughuli za Kiuchumi na Kijamii katika Mazingira

Hii ni Zana Shirikishi inayoiwezesha jamii kubaini athari za shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii katika mazingira. Kwa kufanya zoezi hili, jamii inawezeshwa kuandaa mpango unaozingatia masuala muhimu ya mazingira. Hii ni hatua muhimu katika kuhakikisha kuwa upangaji mipango unazingatia misingi ya maendeleo endelevu.

Shughuli za kiuchumi ni kama ifuatavyo; kilimo, uvuvi, ufugaji, na biashara. Kwa upande wa pili shughuli za kijamii ni kama usafi wa makazi, matumizi ya madawa ya pembejeo, ujenzi na sherehe.

Shughuli kulingana na umuhimu



Chapati kubwa inaonyesha kuwa shughuli husika ina umuhimu mkubwa zaidi kwa Jamii. Katika kielelezo, shughuli za kilimo (kilimo cha mazao na ufugaji), ndizo zenye umuhimu mkubwa zaidi kwa Jamii.

Uhusiano wa shughuli za kiuchumi na kijamii na mazingira mazingira



Chapati iliyo karibu zaidi na kitovu inaonyesha kuwa shughuli husika ina athari kubwa zaidi katika mazingira. Uchambuzi wa Mahusiano baina ya mazingira na shughuli za kiuchumi na kijamii unaweza kufanyika kwa kutumia jedwali kama inavyooneshwa hapa chini.

Mahusiano baina ya Shughuli za Kiuchumi na Kijamii na Mazingira

Shughuli za Kiuchumi/Jamii zenye Athari kwenye Mazingira	**Namna inavyofanyika**	**Athari**	**Ufumbuzi**
Biashara ndogondogo			
Kilimo			
Ufugaji			
Uvuvi			

Ramani ya Umilikaji Rasilimali Kijinsia

Ramani ya Umilikaji Rasilimali Kijinsia ni Zana Shirikishi inayotumika kuwezesha Jamii kubaini mapengo kijinsia juu ya umilikaji, utoaji maamuzi na nguvu kazi katika Kaya. Zana hii inawezesha Jamii kuibua masuala yanayohusu mapengo katika kumiliki rasilimali, mgawanyo wa kazi na majukumu kati ya wanaume, wanawake na watoto. Ramani ya rasilimali kijinsia inasaidia kuainisha mapengo ya kijinsia ili kurekebisha hali hiyo. Ramani hii inasaidia kuamua ni nani anashiriki zaidi katika kazi fulani. Aidha ramani ya rasilimali kijinsia inasaidia kujifunza na kuelewa nani anamiliki na nani anatoa maamuzi, nani anatoa nguvu kazi, na nani anawajibika juu ya rasilimali katika Kaya.

Hatua:

1. Wanakikundi wataje rasilimali muhimu na za kawaida zilizopo kwenye kaya.
2. Waeleze rasilimali moja moja, juu ya jinsi gani ina:-
    - miliki rasilimali
    - inachangia nguvu kazi
    - inatoa maamuzi ya kuzitumia

Kielezo cha Ramani ya Umilikaji Rasilimali Kijinsia

Ng'ombe	**Nyumba**	**Baiskeli**
U M N	U M N	U M N
Wanyama	**Shamba**	
Wadogo wadogo U M N	Mazao ya kudumu U M N	
Radio U M N		

Ufunguo:

U = Umilikaji

M = Maamuzi

N = Nguvu kazi

3. Makundi mahususi yawezeshwe kuainisha na kuchora ramani ya Umilikaji Rasilimali Kijinsia, kama inavyooneshwa hapo chini.

Jedwali 8. Ramani ya Umilikaji Rasilimali Kijinsia

Rasilimali	**Umilikaji**		**Maamuzi**		**Nguvukazi**	
	Me	**Ke**	**Me**	**Ke**	**Me**	**Ke**
Ng,ombe	√		√		√	√
Nyumba	√		√		√	√
Baiskeli	√	√	√		√	√
Sungura/ Kuku	√		√			√
Radio	√		√		√	√
Mazao	√		√		√	√
Jumla:	***6***	***1***	***6***	***0***	***5***	***6***

Jedwali la majumuisho ya ramani ya Umilikaji Rasilimali Kijinsia

	Umilikaji	Maamuzi	Nguvu kazi
KE	1	0	6
ME	6	6	5

4. Makundi mahususi kujadili kama wanaona kuna mapengo kijinsia watoe ushauri au hatua za kuchukua kurekebisha au kuboresha hali iliyopo.

Jedwali 9 Uchambuzi wa mapengo kijinsia

Pengo la kijinsia	Sababisho	Ufumbuzi
Wanaume wanamiliki rasilimali nyingi zaidi kuliko wanawake. Wanaume wana maamuzi zaidi kuliko wanawake	Mila na desturi za kuwagandamiza wanawake Mfumo dume	Elimu ya kijinsia itolewe

Shughuli za Kutwa Kijinsia

Shughuli za kutwa kijinsia ni Zana Shirikishi ambayo inasaidia kuibua mapengo ya kijinsia.Shughuli nyingi katika Jamii zinaongozwa bila kujali jinsia. Hapo awali kulikuwa na shughuli ambazo zilitengwa maalum kwa ajili ya jinsi ya kike kama vile kuchota maji, kutwanga, kupika, kuogesha watoto. Hivi sasa watu wengi wameanza kuona umuhimu wa kuhusisha mipango na kazi ili kusaidiana bila kujali jinsia.

Hata hivyo katika Jamii zingine mgawanyo wa shughuli za jinsia bado unaendelea. Kwa maana hiyo, ni muhimu timu ya Wawezeshaji kuwa makini ili isionekane inaingilia mila na desturi za Jamii hiyo. Kwa upande wa pili ni lazima kuwa makini na kazi maalumu za jinsia ili mipango mipya inayoanzishwa isizidi kugandamiza kundi ambalo tayari linafanyishwa kazi nyingi.

Kuanzisha uhamasishaji katika ukusanyaji wa takwimu kunasaidia Jamii yenyewe kuanza kuangalia, ni wanaume au wanawake wanaofanya kazi nyingi za maendeleo katika mfumo wa mila na desturi zilizopitwa na wakati. Je kuna mabadiliko yoyote mazuri au kushutumu yaliyotokea katika shughuli za wajibu wa jinsia bila kuathiri Jamii. Ni nani aliyeanzisha mabadiliko hayo, Haya ni baadhi ya maswali ambayo wanaKijiji wanapaswa kujiuliza katika zoezi la kukusanya takwimu na hata wakati wa kupanga mipango yao ya baadaye.

Jedwali Na. 10: Shughuli za kutwa kijinsia - Kijiji cha Diola

Muda	Baba	Mama	Mtoto wa kiume	Mtoto wa kike
11.00	Amelala	Ameamka na kutayarisha mlo wa asubuhi	Amelala	Ameamka
11.00 – 12.00	Amelala	Amefuata maji (1)	Amelala	Amefuata maji (1)
12.00 – 01.00	Ameamka	• Anafanya kazi za usafi wa mazingira • Kuchemsha maji ya kuoga • Kuandaa kifungua kinywa (1)	Ameamka	Anasafisha vyombo (1)
01.00 – 01.30	Kifungua kinywa	Kifungua kinywa	Kifungua kinywa	Kifungua kinywa
01.30 – 07.00	Kufanya kazi za shambani (5.30)	Kufanya kazi za shambani(5.30)	Kwenda shule(5.30)	Kwenda shule(5.30)
07.00 – 08.00	Shambani (1)	Anatafuta mboga/ kuni (1)	Shule (1)	Shule (1)
08.00 – 09.00	Kurudi nyumbani (1)	Kurudi nyumbani akiwa na mzigo wa kuni (1)	Kurudi nyumbani (1)	Kurudi nyumbani (1)
09.00 – 10.00	Amepumzika	Anaandaa chakula (1)	Amepumzika	Anamsaidia mama kuandaa chakula (1)
10.00 – 10.15	Anakula	Anakula	Anakula	Anakula
10.30 – 04.00 usiku	Burudani	• Kufua nguo • Kuosha vyombo • Kuangalia mifugo • Kuogesha watoto • Anatandika kitanda (5.30)	Anacheza na kujisomea	Anaosha vyombo na kujisomea (5.30)
04.00 – 11.00 asubuhi	Amelala	Anaanda mlo wa asubuhi (1)	Amelala	Amelala
Masaa ya kufanya kazi	7:30	17	7:30	16

*Namba zilizo kwenye mabano zinaonesha saa za kufanya kazi/shuleni.

Jedwali 11 mapengo kijinsia

Mapengo	Sababisho	ufumbuzi
Mama anafanya kazi nyingi zaidi za nyumbani kuliko baba	Mgawanyo mbaya wa kazi. Mfumo dume	Elimu ya jinsia itolewe

Vyanzo vya Mapato na Matumizi

Hii ni Zana Shirikishi inayowezesha Jamii kuelewa vyanzo vya Mapato na Matumizi ya Halmshauri yao kwa kipindi cha mwaka mmoja. Pia huwezesha kutekeleza,kufuatilia na kufanya tathmini ya mpango wao wenyewe. Inaleta uwazi na utawala bora.

1. Wabunge bongo juu ya vyanzo mbalimbali vya mapato vilivyopo ndani ya Kijiji chao.
2. Waainishe vyanzo vyenye ugumu wa kuvikusanya na nini kifanyike kurekebisha hali hiyo.
3. Waombe wajadili vyanzo vingine ambavyo bado havijashughulikiwa
4. Waweke mikakati ya ukusanyaji wa mapato hayo
5. Wabainishe maeneo ya kupewa kipaumbele kwa ajili ya matumizi ya rasilimali hizo zilizobainishwa.

Jedwali 12: Uainishaji wa vyanzo vya Mapato na Matumizi – Kijiji cha Nrao Kisangara

Vyanzo vya mapato		**Matumizi**	
Vyanzo vya Mapato:		(i) Utawala:	
(i) Vyanzo vya ndani		Gharama za mikutano	100,000
Kodi	1,000,000	WDC	200,000
Ushuru	1,200,000	Uchunguzi na usafiri	500,000
Ada ya vinywaji vya kienyeji	800,000	Shajala	200,000
Mchango wa chakula shuleni	2,000,000	Tukrima	600,000
Ada ya mchanga	2,500,000	Mwenge wa uhuru	500,000
Jumla ndogo:	**7,500,000**	**Jumla ndogo:**	**2,100,000**
(ii) Vyanzo vya nje		(ii) Maendeleo	
Mchango wa Halmashauri		Chakula cha wanafunzi Shule ya msingi	2,000,000
Madarasa 2	1,000,000	Ujenzi wa darasa na nyumba ya walimu (Halmashauri 2,000,000 na Halmashauri ya Kijiji/ Kata	1,000,000 500,000
TASAF	2,000,000		
Jumla ndogo:	**3,000,000**	Zahanati : - TASAF - Halmashauri Kijiji/ Kata	 2,000,000 600,000
(iii) Mapato yasiyokuwa ya fedha		Uzalishaji wa mahindi	1,400,000
Nguvu kazi	1,100,000	Jumla ndogo:	9,500,000
Jumla kuu:	***11,600,000***	***Jumla kuu:***	***11,600,000***

Makadirio ya makusanyo ya mapato kutoka vyanzo mbalimbali huonyesha kiwango cha uwezo wa Kijiji/ Kata kuweza kugharimia baadhi ya miradi yake ya maendeleo.

SIKU YA TANO: Kujadili Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025

Shughuli kuu: Makundi mahususi kujadili Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025

Kuanzia siku ya tano hadi ya saba shughuli kubwa itakuwa ni kujadili Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na kuandaa rasimu yampango wa Jamii. Kazi hii itafanywa na makundi mahususi na malengo yatakayojadiliwa ni yale yaliyochaguliwa katika Mkutano Mkuu wa Uzinduzi wa Mchakato.

Lengo kuu: ***Maisha Bora na Mazuri*.**

Malengo yatakayojadiliwa yanaweza kuwa miongoni mwa haya yafuatayo hapa chini:-

1.1 kujitosheleza kwa chakula na kuwa na uhakika wa upatikanaji wake
1.2 Elimu ya msingi kwa wote.
1.3 Usawa wa kijinsia
1.4 Upatikanaji wa huduma za afya ya msingi kwa watu wote

Malengo

1.1 Kujitosheleza kwa chakula na uhakika wa upatikanaji wake.

Ili kufikia lengo hili vipengele vifuatavyo vitazingatiwa:

- Upatikanaji na matumizi ya zana na pembejeo za kilimo na mifugo
- Uendelezaji mazao ya mifugo – Maziwa, Nyama na Ngozi
- Ubora wa huduma za Ugani katika Kilimo na Mifugo
- Upatikanaji wa ardhi.
- Kilimo cha umwagiliaji maji kutumia mito, maziwa na teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua
- Kilimo cha bustani za mboga na matunda.
- Masoko ya mazao ya ndani na ya nje.
- Barabara za vijijini.
- Huduma za fedha na mikopo vijijini.
- Hifadhi bora ya mazingira – Kilimo mseto, mmomonyoko wa ardhi, makazi, vyanzo vya maji, misitu, wanyama pori
- Usindikaji wa mazao na matunda
- Uhifadhi wa mazao.
- Milo kwa siku katika kaya
- Ulaji wa vyakula vyenye virutubisho

- Hali ya lishe ya watoto 0 – 5
- Pato la kaya
- Zao kuu la biashara
- Ufugaji nyuki na samaki
- Uvuvi katika mito, maziwa, mabwawa na bahari
- Mifugo midogo midogo kama kuku, bata, sungura
- Kuongeza uzalishaji kwa ekari
- Kupambana na wanyama, ndege waharibifu.
- Kupambana na wadudu waharibifu
- Uendelezaji malisho ya mifugo
- Kuzuia magonjwa ya mifugo
- Athari za UKIMWI katika uzalishaji
- Umwagiliaji na upatikanaji wa maji
- Ardhi kwa ajili ya ufugaji na wanyama
- Uzalishaji na afya ya mifugo
- Ardhi kwa ajili ya kilimo na mifugo
- Uzalishaji wa mazao
- Kuhifadhi, kuvuna na kusindika mazao
- Matumizi endelevu ya mali asili
- Uendelezaji wa sekta binafsi ya kilimo
- Athari za VVU/UKIMWI katika kilimo.

1.2 Elimu ya msingi kwa wote, kufuta ujinga na kufikia kiwango kinachoridhisha cha elimu ya kati na juu kulingana na mahitaji ya kuwa na watenda kazi wenye uwezo wa kushughulikia kikamilifu changamoto za kimaendeleo katika ngazi zote

Ili kufikia lengo hili vipengele vifuatavyo vitazingatiwa

(a) Elimu ya Msingi

- Elimu ya awali
- Uwekezaji wa watu binafsi katika elimu ya msingi.
- Elimu ya msingi
- Uandikishaji wa watoto
- Utoro mashuleni
- Usafi na utunzaji wa mazingira mashuleni

- Usafiri kwa wanafunzi
- Wanafunzi kupata chakula cha mchana shuleni
- Kiwango cha kujiunga na elimu ya Sekondari.
- Ubora na uwiano wa matundu ya vyoo
- Madaraja ya waalimu na idadi yao.
- Nyumba za waalimu zilizopo na mahitaji.
- Upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kama uwiano wa kitabu kwa wanafunzi.
- Upatikanaji wa maji salama ya kunywa shuleni
- Umbali wa shule
- Athari za VVU/Ukimwi mashuleni
- Elimu ya watu wazima
- Kiwango cha elimu
- Idadi ya waliojiandikisha kwenye elimu ya watu wazima.
- Idadi ya wanaohudhurio darasa la watu wazima.
- Walimu wa kisomo cha watu wazima – idadi.
- Madarasa ya elimu ya watu wazima – idadi.

Angalizo: Takwimu zichambuliwe kwa kuzingatia jinsia

1.3 Usawa wa kijinsia na kuwapa wanawake kushiriki kikamilifu katika masuala yote ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni

Ili kufikia lengo hili vipengele vifuatavyo vitazingatiwa

- Ili kufikia lengo hili vipingere vifuatavyo vitazingatiwa
- Vituo vya kulelea watoto
- Mahusiano na mapengo ya kijinsia yaliyopo katika Jamii.
- Katika utendaji kazi na mgawanyo wake
- Nafasi za kujiunga na elimu ya ufundi na utaalam mbalimbali wa elimu ya juu.
- Katika umilikaji mali.
- Katika utoaji maamuzi.
- VVU/UKIMWI

- ⇨ Mila na desturi zilizopitwa na wakati katika Jamii
    - Ukeketaji wanawake
    - Miiko ya ulaji wa vyakula mbalimbali
    - Miiko ya utumiaji wa vyoo.
    - Kurithi wajane.
    - Ndoa katika umri mdogo
    - Matumizi ya teknolojia rahisi na sahihi (mikokoteni, majiko sanifu) kwa lengo la kupunguza mzigo wa kazi katika kaya.

1.4 Upatikanaji wa huduma za afya ya msingi kwa watu wote

Ili kufikia lengo hili vipengele vifuatavyo vitazingatiwa;

- ⇨ Magonjwa makuu yanayosumbua/ yanasibu eneo hilo kama Malaria, Kuharisha, Vichomi, Upungufu wa damu.
- ⇨ Magonjwa ya mlipuko, kama kipindupindu, Surua, Uti wa mgongo.
- ⇨ Magonjwa ya kuambukiza kama Kifua kikuu, UKIMWI, Magonjwa ya ngono.
- ⇨ Huduma za afya ya Msingi zinazopatikana.
    - Sanduku la huduma ya kwanza.
    - Zahanati (za binafsi, mashirika, serikali, Taasisi)
    - Kituo cha afya (za binafsi, mashirika, serikali, Taasisi).
    - Hospitali (za binafsi, mashirika, serikali, Taasisi)
    - Hospitali ya rufaa.
    - Huduma ya ushauri nasaha na upimaji virusi vya UKIMWI

- ⇨ Wastani wa umbali ilipo huduma ya afya. Idadi ya watu wanaohudumiwa na huduma ya afya iliyopo.
- ⇨ Uwiano wa watoa huduma ya afya na wananchi kama Daktari, Muuguzi mkunga.
- ⇨ Elimu ya afya kwa Jamii.
    - Matumizi ya vyoo
    - Usafi wa mazingira ya kaya
    - Kuchemsha maji ya kunywa
    - Usafi wa mwili na mavazi

SIKU YA SITA: Kujadili Dira ya Taifa ya Maendeleo

Shughuli kuu: Makundi mahususi yanaendelea kujadili Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025

Malengo yatakayojadiliwa yanaweza kuwa miongoni mwa haya hapa chini:-

1.5 Upatikanaji wa huduma bora za uzazi kwa watu wote wenye umri unaostahili.

1.6 Kupunguza vifo vya watoto wachanga na vifo vya uzazi kwa robo tatu ya viwango vya sasa.

1.7 Upatikanaji wa maji salama kwa watu wote.

1.8 Kuongeza wastani wa umri wa kuishi kulingana na kiwango kilichofikiwa na nchi zenye mapato ya kati.

1.9 Kuondoa kabisa umasikini uliokithiri.

1.5 Upatikanaji wa huduma bora za uzazi kwa watu wote wenye umri unaostahili.

Ili kufikia lengo hili vipengele vifuatavyo vitazingatiwa

- ⇨ Kunyonyesha watoto miezi sita mfululizo bila vyakula vya kulikiza
- ⇨ Haki ya kupata chanjo kwa wanawake walio katika umri unaostahili kuzaa TT2+
- ⇨ Chumvi yenye madini joto
- ⇨ Chanjo kwa wanawake wajawazito (TT1 na TT2 na kuendelea dawa za minyoo na ferrous). Baada ya kujifungua (ferrous na nyongeza ya vitamin A)
- ⇨ Huduma za uzazi zilizopo
    - za asili.
    - za kisasa
- ⇨ Wahudumu wa afya ya uzazi.
    - MCHA/ PHN
    - Wakunga wa jadi, waliopata mafunzo na ambao hawajapata mafunzo.
    - Wahudumu wa uzazi wa mpango.
- ⇨ Njia za uzazi wa mpango zinazotumika
- ⇨ Matumizi ya fomu za ufuatiliaji za wamama wajawazito.
- ⇨ Umbali huduma ya uzazi inakopatikana.
- ⇨ Huduma za kutembelewa kaya/ Kijiji.
- ⇨ Viwango vya kukubalika na kutumia huduma za uzazi wa mpango.
- ⇨ Elimu ya uzazi salama kwa wanawake na wanaume.
- ⇨ Upatikanaji wa maji safi.

1.6 Kupunguza vifo vya watoto wachanga na vifo vya uzazi kwa robo tatu ya viwango vya sasa.

Ili kufikia lengo hili vipengele vifuatavyo vitazingatiwa

- ⇨ Kunyonyesha watoto wachanga kwa miezi sita bila vyakula vya kulikiza
- ⇨ Idadi ya vifo vya watoto wachanga chini ya mwaka mmoja.
- ⇨ Idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano.
- ⇨ Idadi ya wanawake wanaozaa wakiwa na umri chini ya miaka 19 na wale wanaozaa zaidi ya miaka 35
- ⇨ Hali ya lishe kwa watoto chini ya miaka mitano.
    - Utapiamlo mkali.
    - Utapiamlo wa kati.
    - Hali nzuri.
- ⇨ Chanjo kwa watoto chini ya miaka mitano.
    - BCG
    - Polio
    - Dondakoo
    - Pepopunda
    - Surua
    - Vitamin A nyongeza.
    - Kifaduro na Hepatitis
- ⇨ Uendeshaji wa siku ya mtoto wa Kijiji/ Kata
- ⇨ Matumizi ya fomu za upimaji na ufuatiliaji wa maendeleo ya mtoto.
- ⇨ Elimu juu ya huduma ya Kinga na Matibabu sahihi ya magonjwa ya watoto.
- ⇨ Watoto wanaozaliwa na uzito pungufu.
- ⇨ Watoto wanaozaliwa kabla ya wakati.
- ⇨ Watoto wanaozaliwa wakiwa wafu.
- ⇨ Idadi ya vifo vya akina mama wanaokufa wakati wa kujifungua.
- ⇨ Huduma za akina mama wajawazito.
    - Wakati wa ujauzito
    - Wakati wa kujifungua
    - Baada ya kujifungua.
    - Rufaa ya wajawazito
- ⇨ Malezi na matunzo ya akina mama wajawazito na watoto.
- ⇨ Ufuatiliaji wa taarifa za fomu za klinic kwa wanandoa, mke na mume.
- ⇨ Matumizi ya chumvi yenye madini joto

1.7 Upatikanaji wa maji safi na salama kwa watu wote.

Ili kufikia lengo hili vipengele vifuatavyo vitazingatiwa

- Vyanzo vya maji kwa watu wote.
- Chemchem
- Mabwawa/ lambo
- Visima vya asili
- Mito
- Visima vifupi.
- Visima virefu vyenye pampu za dizeli; umeme; upepo.
- Uvunaji wa maji ya mvua.
- Pampu za mkono
- Pampu za dizeli, upepo
- Hydram na umeme

⇨ Uhakika wa upatikanaji wa maji; wakati wote au wa msimu

⇨ Idadi ya watu wanaopata huduma ya maji katika umbali usiozidi mita 400 vijijini.

⇨ Kaya zenye huduma ya maji majumbani.

⇨ Fursa za upatikanaji wa maji zisizotumika.

⇨ Uelewa wa Jamii kuhusu kunywa maji yaliyochemshwa.

⇨ Uhai wa kamati ya maji

- Muundo unaozingatia jinsia
- Mfuko wa maji
- Mahusiano ya kamati ya maji na Halmashauri ya Kijiji
- Wahudumu wa Jamii wa miradi ya maji
- Wahudumu wenye ujuzi/ wasio na ujuzi
- Vyoo na tabia ya usafi katika Kaya

1.8 Kuongeza wastani wa umri wa kuishi kulingana na kiwango kilichofikiwa na nchi zenye mapato ya kati.

Ili kufikia lengo hili vipengele vifuatavyo vitazingatiwa

- ⇨ Kuongeza kipato na uwezo wa kujikimu katika kaya.
- ⇨ Lishe bora
    - Kuzalisha na kula vyakula vyenye virutubisho vya kutia mwili nguvu kujenga na kuulinda mwili (chakula bora) nafaka, kunde, nyama, samaki, mayai, maziwa, mboga.
    - Lishe za watoto wenye umri wa miaka 0 – 5.
    - Matumizi ya chumvi yenye madini joto.
- ⇨ Elimu ya Afya ya msingi
    - Usafi wa mazingira ya makazi, nyumba bora na matumizi ya vyoo.
    - Usafi na usalama wa maji ya kunywa.
    - Elimu juu ya huduma za kinga na kutibu kikamilifu maradhi.
    - Kushiriki mazoezi ya viungo, michezo na burudani.
- ⇨ Uelewa wa Jamii juu ya virusi vinavyosababisha UKIMWI
    - Maana ya UKIMWI
    - Njia za maambukizo ya virusi
    - Dalili za mtu mwenye UKIMWI
    - Namna ya kujikinga
    - Huduma za waathirika wa UKIMWI
    - Nyumba bora
    - Utunzaji mazingira – kutunza vyanzo vya maji, misitu
- ⇨ Upatikanaji wa ubora wa huduma za msingi
    - Afya
    - Elimu
    - Maji
    - Barabara
    - Nishati
- ⇨ Mipango ya matumizi bora ya ardhi
    - Upimaji wa makazi mijini
    - Kutenga maeneo ya makazi
    - Shughuli za uchumi na huduma za Jamii mijini na vijijini
    - Mgawanyo wa ardhi kwa vijana kwa kuzingatia jinsia
- ⇨ Ulinzi na Usalama
    - Udhibiti wa ajali
    - Kujianda kukabiliana na maafa na dharura
    - Kudhibiti mauaji na uhalifu mwingine kama vile ubakaji, ujambazi, uuaji wa vikongwe.
    - Kujenga maadili mema kwa vijana

1.9 Kuondoa kabisa umasikini uliokithiri

Umaskini uliokithiri unaweza kuangaliwa katika vipengele vifuatavyo

- ★ Chakula, Mavazi na Malazi
- ★ Wastani mdogo wa umri wa kuishi
- ★ Kiwango kikubwa cha watoto wenye utapiamlo
- ★ Kiwango kikubwa cha utegemezi wa vijana wazee, na kaya kubwa

Ili kufikia lengo hili vipengele vifuatavyo vitazingatiwa

- ★ Kuongeza uwezo wa kujikimu katika kaya
- ★ Kuongeza wastani wa kuishi
- ★ Kupunguza utapiamlo kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka 5
- ★ Kupunguza vifo vya watoto walio na umri wa chini ya miaka 5
- ★ Kujenga mazingira yanayowezesha vijana kujiajiri na kuendeleza stadi za kazi.
- ★ Uanzishaji wa vikundi vya uzalishaji
- ★ Upatikanaji wa mikopo
- ★ Vikundi vya kuweka na kukopa
- ★ Kuwezesha kupata na kutumia ardhi
- ★ Vijana kushiriki katika kutoa maamuzi
- ★ Mafunzo ya ufundi na stadi za kazi
- ★ Ushirikishwaji wa Jamii katika kupanga na kutoa maamuzi
- ★ Kuwakwamua watoto walioko kwenye mazingira magumu
- ★ Ajira mbaya za watoto
- ★ Watoto wanaoongoza kaya
- ★ Watoto wanaonyanyaswa
- ★ Watoto waliotelekezwa

SIKU YA SABA: Kujadili Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025

Shughuli kuu: Makundi mahususi Kujadili Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025

Lengo la pili katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambalo ni **Uongozi Bora na Utawala wa Kisheria** litajadiliwa. Malengo yatakayo jadiliwa yanaweza kuwa miongoni mwa haya yafuatayo hapa chini:

2.1. Maadili mema na kuthamini utamaduni

2.2 Uadilifu na kuheshimu utawala wa sheria

2.3 Kutokuwepo rushwa na maovu mengine

2.4 Jamii iliyoelimika na inayojiamini, inayojifunza kutokana na uzoefu wake na wa wengine na yenye kumiliki na kubaini agenda ya maendeleo yake.

2.1 Maadili mema na Kuthamini Utamaduni.

Ili kufikia lengo hili vipengele vifuatavyo vitazingatiwa

- Uendelezaji wa mila nzuri katika Jamii
- Kufanya kazi kwa bidii na maarifa stadi za kazi mbalimbali
- Utunzaji wa familia
- Kuheshimiana kwa watu wa rika na jinsi zote
- Kusaidia wasio jiweza hasa, vikongwe na watoto walio kwenye mazingira magumu.

2.2 Uadilifu na kuheshimu utawala wa sheria.

Ili kufikia lengo hili vipengele vifuatavyo vitazingatiwa

- Kuheshimu haki za binadamu
- Haki ya kuishi na kulindwa
- Haki ya uhuru wa mawazo
- Haki ya kufanya kazi
- Haki ya kuheshimiwa na kuthaminiwa utu wake
- Haki ya kutoa maamuzi
- Usawa wa watu wote mbele ya sheria
- Haki ya kuabudu
- Na nyinginezo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

⇨ kuheshimu haki na usawa wa raia

- ⇨ Wajibu wa raia kwa taifa
    - Kushiriki shughuli za maendeleo
    - Kushiriki shughuli za ulinzi wa taifa
    - Kulipa kodi mbalimbali za serikali
    - Kutii sheria za nchi
    - Kuwepo kwa uongozi uliowekwa madarakani kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.
    - Halmashauri ya Kijiji
- ⇨ Muundo wa Halmashauri ya Kijiji na Uongozi wa Vitongoji kama umezingatia kanuni.
- ⇨ Uendeshaji wa Halmashauri ya Kijiji kama unazingatia kanuni na taratibu zilizowekwa.
    - Kufanyika kwa mikutano ya Halmashauri ya Kijiji na Kamati ya Maendeleo ya Kata
    - Utoaji wa taarifa mbalimbali kwa uwazi na ukweli.
- ⇨ Kuwepo sheria ndogo na matumizi yake.

2.3 Kutokuwepo Rushwa na Maovu mengine

Ili kufikia lengo hili vipengele vifuatavyo vitazingatiwa

- Kutekeleza na kufikia malengo ya mipango ya Jamii
- Hifadhi ya usafi wa mazingira
- Kuheshimu sheria na sheria ndogo
- Kutokujenga kwenye maeneo ya wazi na yaliyotengwa kwa huduma za Jamii
- Kutoharibu vyanzo vya majikwa kukata miti, kuchoma mkaa, kuchoma moto, kuchafua mazingira.
- Kupungua kwa gharama za utawala kutokana na udhibiti mzuri wa matumizi wa mapato ya Halmashauri ya Kijiji
- Kuongezeka kwa ukusanyaji wa kodi na mapato mengine ya Halmashauri ya Kijiji
- Kuheshimika kwa mamlaka ya Kijiji
- Kuzingatia kalenda ya vikao na kutoa taarifa za ukweli na uwazi juu ya shughuli mbalimbali za Kijiji
- Kuwepo kwa uwazi katika kutoa huduma
- Uharaka katika kutoa maamuzi
- Ugawaji wa fursa za maendeleo kama ugawaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na mashamba

2.4 Jamii iliyoelimika na inayojiamini, inayojifunza kutokana na uzoefu wake na wengine na yenye kumiliki na kubaini agenda ya maendeleo yake.

Ili kufikia lengo hili vipengele vifuatavyo vitazingatiwa:

- Jamii inaelewa haki na wajibu wake
- Jamii inashiriki katika maamuzi ya upangaji na utekelezaji wa shughuli za maendeleo
- Jamii ina uwezo wa kugharimia huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi
- Wepesi wa kukubali mabadiliko na kuiga teknolojia mpya
- Kuwapo mipango ya kuelimisha Jamii

SIKU YA NANE: Kuandaa Rasimu ya Mpango

Shughuli kuu: Makundi mahususi kuandaa Rasimu ya Mpango

Katika siku ya nane, Afisa Mtendaji wa Kijiji kwa kushirikiana na makundi mahususi wataandaa Rasimu ya Mpango.

Rasimu ya Mpango itaandaliwa kwa kuzingatia takwimu zilizokusanywa kwa kutumia Zana Shirikishi na majadiliano ya makundi mahususi juu ya Dira ya Taifa 2025. Hivyo, itajumuisha mambo yafuatayo:

- Nini Jamii inataka kufikia (malengo mahususi)
- Rasilimali/Taasisi ambazo zikitumika ipasavyo zitawezesha kufikia malengo yanayotarajiwa (Fursa)
- Vipingamizi vya matumizi ya Fursa (Vikwazo),
- Sababu za kuwepo kwa Vikwazo (sababisho)
- Hatua za kuchukua ili kuonkoa Vikwazo (ufumbuzi)
- Shughuli zitakazolenga kuondoa Vikwazo (hatua za utekelezaji)
- Rasilimali zitakazohitajika wakati wa utekelezaji (mahitaji)
- Makadirio ya gharama- Jamii inaweza kufanya nini na haiwezi kufanya nini ili kufikia hatua za utekelezaji(gharama)
- Njia zitakazotumika kupima mafanikio (viashiria)

JEDWALI 13 MFANO WA RASIMU YA MPANGO SHIRIKISHI JAMII ILIYOANDALIWA NA MAKUNDI MAHUSUSI:

Lengo Mahsusi	**Fursa**	**Vikwazo**	**Sababisho**	**Ufumbuzi**	**Hatua za utekelezaji**	**Mahitaji**	**Gharama**		**Viashiria**
							Ndani	**Nje**	
Kuongeza uzalishaji wa mahindi kutoka gunia 10 kwa sasa hadi gunia 15 kwa ekari ifikapo mwaka 2010	Upatikanaji/kuwepo kwa pembejeo za kilimo(mbegu, mbolea na dawa za kuulia wadudu	Uelewa Mdogo juu ya Matumizi ya Pembejeo za kilimo	Upungufu wa huduma za ugani	Uboreshaji wa matumizi ya pembejeo za kilimo	Kupatikana kwa usafiri	Pikipiki, Mafuta, Oili,		1,150,000 50,000	Idadi ya magunia ya mahindi yanayozalishwa kwa ekari
					Kuunda vikundi vya shughuli za kilimo katika vitongoji				
					Kutayarisha mashamba darasa	Mbegu Posho ya Mtaalamu	50,000	75,000	
					Kutoa mafunzo ya utengenezaji wa mboji (mbolea)	- Mbolea -Maji -Majani	0	0	

SIKU YA TISA: Mkutano wa Halmashauri ya Kijiji

Shughuli kuu: Kufanya Mkutano wa Halmashauri ya Kijiji

Mkutano maalum wa Halmashauri ya Kijiji utaitishwa ili kuweka vipaumbele na kundaa Rasimu ya Mpango wa miaka mitatu, kabla ya kuupeleka kwenye mkutano wa Kamati ya Maendeleo ya Kata na Mkutano Mkuu wa Kijiji.

Madhumuni ya mkutano wa Halmashauri ya Kijiji

Kupokea na kujadili malengo, fursa, vikwazo, sababisho, na njia za ufumbuzi kama ilivyojitokeza katika makundi mahususi ili kuandaa Mpango Shirikishi wa Kijiji. Wawakilishi wa makundi mahususi watakaribishwa kushiriki katika kikao hiki.

Hatua:

1. Mwenyekiti wa kijjij atafungua mkutano.
2. Afisa Mtendaji wa Kijiji ataelezea hatua zote za Mchakato.
3. Afisa Mtendaji wa Kijiji akishirikiana na Wawezeshaji wa Jamii watawasilisha Rasimu ya Mpango kwa utaratibu ufuatao:
   - Takwimu za awali za Kijiji
   - Ramani ya Kijiji na kataa ya njia
   - Uchambuzi wa Taasisi
   - Ramani ya Umilikaji Rasilimali Kijinsia
   - Uchambuzi wa shughuli za kutwa kijinsia
   - Kalenda ya msimu
   - Matukio ya kihistoria
   - Tathmini ya uwezo wa kujikimu wa kaya
   - Vyanzo vya Mapato na Matumizi
   - Rasimu ya Mpango (Malengo, Malengo mahsusi, fursa, vikwazo, sababisho, ufumbuzi, hatua za utekelezaji, mahitaji na gharama)
4. Halmachauri ya Kijiji itaweka vipumbele vya malengo mahususi. Ikumbukwe kwamba malengo yote mahususi yatalinganishwa kwa pamoja

Kuweka Vipaumbele

Jebwali: 14 Mlinganisho kijozi

Lengo mahususi	Kuongeza uzalishaji wa mahindi	Kuongeza uandikishaji shuleni	Kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama	Kuongeza pato la kaya	Alama	Nafasi (kipaumbele)
Kuongeza uzalishaji wa mahindi		Kuongeza uzalishaji wa mahindi	Kuongeza uzalishaji wa mahindi	Kuongeza uzalishaji wa mahindi	3	1
Kuongeza uandikishaji shuleni			Kuongeza uandikishaji shuleni	Increased household income	1	3
Kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama				Kuongeza pato la kaya	0	4
Kuongeza pato la kaya					2	2

Mwisho kila lengo mahususi huhesabiwa na kuwekwa alama. Kisha kila moja hupewa nafasi kuanzia ya kwanza hadi mwisho. Kwa mfano huu kipaumbele cha kwanza kwa mlinganisho kijozi ni Kuongeza uzalishaji wa zao la Mahindi ndio lengo mahususi la kufikia shabaha ya kujitosheleza kwa chakula.

5. Baada ya kuweka vipaumbele Halmashauri ya Kijiji huandaa Rasimu ya Mpango wa miaka mitatu. Idadi ya malengo mahususi itategemea upatikanaji wa rasilimali za ndani na za nje kwa kuzingatia yafuatayo:
    - Malengo ambayo utekelezaji wake unahitaji rasilimali kutoka nje yasizidi kumi(10)
    - Malengo yote ambayo utekelezaji wake hauhitaji rasilimali za nje yanaweza kujumuishwa.

Kuandaa Rasimu ya Mpango wa Miaka Mitatu

Jedwali 15 mfano wa Rasimu ya Mpango wa miaka 3

Rasimu ya Mpango wa miaka 3 ya mwaka 2007. Kijiji _____ Kata _____ Wilaya _____ Mkoa_____								
kipaumbele	Malaengo mahususi	Hatua za utekelezaji	**Mwaka 1**		**Mwaka 2**		**Mwaka 3**	
			Kijiji kinaweza kufanya	Kijiji hakiwezi kufanya	Kijiji kinaweza kufanya	Kijiji hakiwezi kufanya	Kijiji kinaweza kufanya	Kijiji hakiwezi kufanya

6. Halmashauri ya Kijiji itaainisha vyanzo vya Mapato na Matumizi
7. Halmashauri ya Kijiji itaandaa Rasimu ya Mpango wa miaka mitatu, ambao utawasilishwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji katika mkutano wa kamati ya maaendeleo ya Kata.

SIKU YA KUMI: Mkutano Maalum wa Kamati ya Maendeleo ya Kata

Shughuli kuu: Mkutano maalum wa Kamati ya Maendeleo ya Kata

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Kata ataitisha mkutano ili mipango ya Halmashauri za vijiji iwasilishwe kwenye Kamati. Kazi kubwa ya Kamati ya Maendeleo ya Kata ni kutoa ushauri wa kitaalamu na inapobidi kuratibu mipango ya vijiji ambayo itatekelezwa na vijiji kwa pamoja. Kwa mfano, ujenzi wa Shule ya Sekondari kwenye Kata.

Ni muhimu kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji kunukuu mapendekezo/ ushauri utakaotolewa na Kamati ya Maendeleo ya Kata ili Rasimu ya Mpango wa Kijiji iboreshwe ipasavyo

SIKU YA KUMI NA MOJA: Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji

Shughuli kuu: Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji

Mwenyekiti wa Kijiji ataitisha Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji kupokea, kujadili na kupitisha mpango.

Yafuatayo ni mambo muhimu ya kuzingatia:

- Mwenyekiti wa Kijiji atafungua mkutano na kueleza madhumuni yake.
- Afisa Mtendaji wa Kijiji akishirikiana na Wawezeshaji wa Jamii wataelezea hatua zote zilizopitiwa wakati wa kupanga.
- Mwenyekiti wa Kijiji atamkaribisha afisa mtendaji kuwasilisha Rasimu ya Mpango wa miaka mitatu.
- Mwenyekiti atawaruhusu wajumbe kujadili mpango kwa uhuru.
- Baada ya majadiliano mwenyekiti awaulize wajumbe kama wameupokea mpango. Kama wameupokea basi uandikwe kwenye karatasi za manila na kubandikwa kwenye sehemu za matangazo.
- Afisa Mtendaji wa Kijiji aorodheshe wote watakaohudhuria kwenye mkutano.
- Afisa mtendji waKijiji ataandika vizuri mpango pamoja na muhtasari wa mkutno mkuu maalum, tayari kwa kuwasilisha kwa Mkurugenzi mtendaji wa Wilaya. Mpango huo utaambatanishwa na Takwimu zilizokusanywa wakati wa Mchakato.

SIKU YA KUMI NA MBILI: Muhtasari wa Shughuli za Utekelezaji

Shughuli kuu: Kuandaa Muhtasari wa Shughuli za utekelezaji kisekta ngazi ya Kata

Baada ya mipango ya vijiji kuidhinishwa, shughuli ya mwisho itakuwa ni kuunganisha mipango hiyo kisekta. Shughuli za utekelezaji za kila sekta zitaunganishwa. Kazi hii itafanywa na Afisa Mtendaji wa Kata akishirikiana na maafisa wengine ngazi ya Kata. Ikiwezekana maafisa watendaji wa vijiji husika washirikshwe. Muhtasari wa shughuli za utekelezaji kisekta utajazwa katika fomu rahisi kama inavyoonekana katika mfano hapo chini. Safu-wima ya mahitaji iachwe wazi itajazwa katika ngazi ya Halmashauri.

Jedwali 15: Mfano wa muhutasari wa shughuli za utekelezeji kisekta

(Muhtasari unaandaliwa katika ngazi ya Kata)

Kata: Chalinze Wilaya: Bagamoyo

Mkoa: Pwani

Sekta: Kilimo (506)…….

Jina la Kijiji	Hatua za Utekelezaji				Mahitaji		
	Kuanzisha mashamba darasa	Kujenga mtandao wa umwagiliaji	Kuajiri wataalamu wa kilimo	Kutoa elimu ya utunzaji wa chakula			
Chahua	3	2	--	✓			
Pingo	4	1	--	✓			
Pera	5	3	--	✓			
Mdaula	4	1	--				
Msolwa	3	--	1	✓			
Chamakweza	3	--	--	✓			
Bwilingu	2	2	1				

KIAMBATISHO I: FOMU YA TAKWIMU

1.0 UTAWALA

1. Kata/Kijiji …….
2. Eneo…….
3. Idadi ya Vitongoji/Mitaa/Vijiji …….
4. Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji: me……. Ke ……
5. Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kata: me……ke……
6. Idadi ya wakazi:
   - Wanawake ……
   - Wanaume …….
   - Wenye uwezo wa kafanya kazi me……ke…….
   - Watoto: me……ke……
   - Yatima: me……ke…….
   - Watoto wa mtaani me…….ke…….
   - Walemavu: me……ke…….
   - Wajane ……
   - Vikongwe me ……..ke……..

2.1 ELIMU YA MSINGI

- Idadi ya watoto wote katika Kijiji/kata wenye umri wa miaka 7 - 13
  Wasichana……., wavulana…….. Jumla…….
- Idadi ya wanafunzi walioacha shule(miaka 3 iliyopita)
  Wasichana……., wavulana…….. Jumla…….
- watoto wa umri wa miaka 7 waliostahili kuandikishwa(miaka 3 iliyopita)
  Wasichana……., wavulana…….. Jumla…….
- wanafunzi wa umri wa miaka 7 walioandikishwa(miaka 3 iliyopita)
  Wasichana……., wavulana…….. Jumla…….
- Wastani wa mahudhurio ya wanafunzi shuleni kwa mwaka(miaka 3 iliyopita)
  Wasichana……., wavulana…….. Jumla…….
- Kiwango cha umalizaji shule ya msingi(miaka 3 iliyopita)
  Wasichana……., wavulana…….. Jumla…….
- Kiwango cha kufaulu(miaka 3 iliyopita)
  Wasichana……., wavulana…….. Jumla…….
- Kiwango cha kujiunga na Elimu ya sekondari(miaka 3 iliyopita)
  Wasichana……., wavulana…….. Jumla…….
- Idadi ya wanafunzi kwa chumba cha darasa…… upungufu wa madarasa uliopo……..
- Idadi ya mikondo……..
- Uwiano wa matundu ya choo me……../ke…….upungufu wa matundu ya vyoo ke……../me……..
- Idadi ya shule za msingi,……. Shule za sekondari……., Vyuo…….
- Nyumba za walimu zilizopo…… na mahitaji……
- Uwiano wa dawati kwa mwanafunzi……upungufu wa madawati…….

- Upatikaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kama uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi……..
- Shule za awali zilizopo……..

2.2. ELIMU YA WATU WAZIMA:

- Elimu inayotolewa(KCK, KCM, MEMKWA, MUKEJA)…….
- Idadi ya waliojiandikisha kwenye Elimu ya watu Wazima
  Me…….. ke……Jumla……
- Idadi ya wanaohudhuria darasa la Watu Wazima
  Me……ke ……Jumla……..
- Walimu wa kisomo cha watu wazima – idadi……..
- Madarasa ya Elimu ya watu wazima - Idadi ……..
- Madarasa ya MEMKWA yaliyoanzishwa……..
  na idadi ya wanafunzi ……me…../ke…… waliojiandikisha

2.0 AFYA

- Magonjwa makuu yanayosumbua taja magonjwa na idadi
  Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……
  Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……
  Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……
  Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……
  Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……
- Magonjwa ya mlipuko taja kama yalitokea na idadi (mwaka 1 uliopita)
  Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……
  Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……
  Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……
  Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……
  Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……
- Magonjwa ya kuambukiza taja magonjwa na idadi kwa <5 na >5

Chini ya miaka 5

Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……
Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……
Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……
Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……
Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……

Zaidi ya miaka 5

Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……
Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……
Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……
Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……
Ugonjwa…….. idadi ya waliougua……

- Huduma za afya zinazopatikana na umbali uliopo kutoka kwa Jamii:
  - Zahanati……umbali…….
  - Kituo cha afya……..umbali…….
  - Hospitali ……..umbali…….
  - Zahanati za Binafsi…… umbali…….
- Uhai wa kamati ya Afya
- Idadi ya vyoo bora……
- Idadi ya wahudumu wa afya ya msingi katika Kijiji…….
- Siku ya afya inavyoendeshwa Kijijini
- Huduma ya kutembelewa Kaya

3.1. HUDUMA BORA ZA UZAZI:

- Idadi ya watoto chini ya mwaka 1
- Idadi ya watoto chini ya miaka 5……..
- Hali ya lishe ya watoto chini ya miaka 5
  - Utapiamlo mkali(idadi)…….
  - Utapiamlo wa kati(idadi……
- Chanjo kwa watoto chini ya mwaka mmoja (waliostahili kuchanjwa na waliopata chanjo)
  - BCG(idadi)……
  - Polio 3(idadi)……
  - Donda koo na Pepopunda (DPT - HB3) (idadi)……
  - Surua(idadi)……
  - Vitamin A(idadi)……
- Idadi ya watoto waliozaliwa na uzito pungufu (mwaka 1 uliopita) (idadi)……..
- Idadi ya watoto waliozaliwa kabla ya wakati (mwaka 1 uliopita) (idadi)……
- Watoto wanaozaliwa wafu (mwaka 1 uliopita) (idadi)……
- Idadi ya vifo vya akina Mama vinavyotokana na uzazi (mwaka 1 uliopita) (idadi)……
- Idadi ya wanawake wanaostahili kuzaa (19-45)……..
- Idadi ya wanawake wanaozaa chini ya umri wa miaka (20) na zaidi ya miaka 35 (mwaka 1 uliopita)……
- Idadi ya waliopata chanjo (TT1) na kuendelea (mwaka1uliopita)……..
- Huduma za uzazi zilizopo
- Idadi ya wanaotumia uzazi wa mpango
- Idadi ya wahudumu wa Afya ya Uzazi:
  - Wakati wa ujauzito
  - Wakati wa kujifungua
  - Baada ya kujifungua

3.2. UKIMWI:

- Vifo vilivyosababishwa na UKIMWI (mwaka 1au 3 iliyopita)idadi……
- Idadi ya waathirika – HIV (waliopimwa)……
- Kiwango cha maambukizo ya UKIMWI

3.0 UPATIKANAJI WA MAJI SAFI NA SALAMA:

- Vyanzo vya maji - orodhesha idadi ya visima, bomba, vyanzo vya
- maji vya asili
- Maji ya kutega: Idadi ya watu wenye visima vya maji ya kutega
- Umbali hadi kwenye vyanzo vya maji
- Idadi ya kaya zinazopata maji safi na salama
- Kamati za maji
- Mfuko wa maji

5.0. HALI YA KIUCHUMI:

- Wastani wa kipato kwa mwaka kwa:
    - Mtu……
    - Kaya……..
    - Mtaa/Kijiji…….
    - Kata…….
- Shughuli kuu za kujiletea kipato(taja)
- Taasisi zilizopo kwenye Kata/Kijiji(mwaka 1 uliopita))

5.1. HUDUMA ZA KIUCHUMI:

- Barabara; taja urefu km……
- Vyanzo vya nishati (taja)
- Mawasiliano
    - wanaotoa huduma ya mawasiliano ya simu za mkononi
    - huduma za posta.
    - Simu za mezani.
    - Tovuti
    - Radio
    - Nukushi
    - Mtandao
    - Televisheni
- Soko la bidhaa na mazao
- Eneo la soko
- Huduma ya usafiri wa umma.

6.0. SEKTA BINAFSI

- Karakana za Ufundi/Gereji
- Viwanda vidogo
- Hotel/Migahawa
- Maduka
- Maduka ya madawa
- Vituo vya mafuta
- Vikindi vya uzalishaji
- Mashirika yasiyokuwa yaSerikali (NGOs)

7.0. KILIMO NA MIFUGO

- Eneo linalofaa kwa kilimo (ekari) …….
- Eneo linalolimwa Ha …….. (kwa kila zao)
- Mazao makuu ya chakula (taja)
- Wastani wa mavuno kwa (ekari) ……. (magunia)
- Mazao makuu ya biashara (taja)
- Upatikanaji wa pembejeo za kilimo na mifugo
- Idadi ya vyama vya ushirika vya wakulima
- Idadi ya iwanda vidogo vya kusindika mazao ya kilimo na mifugo
- Hifadhi ya mazao (maghala, vihenge)
- Idadi ya wafugaji
- Idadi ya mifugo
- Aina ya mifugo
- Eneo linalofaa kwa ufugaji ekari …….
- Magonjwa ya mifugo
- Idadi ya majasho
- Minada
- Idadi ya wataalamu wa kilimo na mifugo

8.0. MAZINGIRA:

Eneo la misitu Ekari …….

Idadi ya miti iliyopandwa……

Idadi ya bustani za miche ya miti……..

KIAMBATISHO II: RATIBA YA MCHAKATO WA KIJIJINI

Siku ya Kwanza

- Maandalizi ya Jamii
  - Kukutana na wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji
  - Kutoa maelezo juu historia ya upangaji mipango ya Jamii
  - Kutoa maelezo ya upangaji mipango ya Jamii kwa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo
  - kujadili na kukubaliana mbinu za kufanikisha mahudhurio ya Mkutano Mkuu
  - kuhamasisha vikundi vya kuhamasisha Jamii
- Kukusanya takwimu

Siku ya pili

- Maandalizi ya Jamii (mwendelezo wa shughuli ya siku ya kwanza).
- Kuendelea kukusanya takwimu.

Siku ya tatu

- Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji wa Uzinduzi wa Mchakato wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo.
- Kuunda Makundi Mahsusi.
  - Wazee wa kike na wa kiume
  - Vijana wa kike na wa kiume
- Kuchagua wachora ramani.
- Kuchagua Wawezeshaji wa Jamii (wawili kutoka kila Kitongoji)
- Kuchora Ramani ya Kijiji
- Kufanya tahmini ya uwezo wa kujikimu wa kaya.

Siku ya nne

- Kataa ya njia
- Matukio ya kihistoria
- Ramani ya Umilikaji Rasilimali Kijinsia.
- Uchambuzi wa Taasisi
- Uchambuzi wa shughuli za kijamii na kiuchumi katika mazingira
- Kalenda ya msimu.
- Uchambuzi wa vyanzo vya Mapato na Matumizi
- Shughuli za kutwa kijinsia.

Siku ya tano

- Makundi Mahsusi kujadili Dira ya Taifa ya maendeleo 2025

Lengo kuu: Maisha Bora na mazuri

- Kujitosheleza kwa chakula na kuwa na uhakika wa upatikanaji wake
- Elimu kwa wote
- Usawa wa kijinsia
- Upatikanaji wa huduma ya Afya ya msingi kwa wote

Siku ya Sita

- Makundi Mahsusi kuendelea kujadili Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025
  - Upatikanaji wa Huduma bora za uzazi kwa wote wenye umri unaostahili.
  - Kupunguza vifo vya watoto wachanga kwa robo tatu ya viwango vya sasa.
  - Upatikanaji wa maji safi na salama kwa watu wote
  - Kuongeza wastani wa umri wa kuishi kulingana na kiwango kilichofikiwa na nchi zenye mapato ya kati.
  - Kuondoa kabisa umasikini uliokithiri.

Siku ya Saba

- Makundi kujadili Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 (Uongozi bora na Utawala wa kisheria)
  - Maadili mema na kuthamini utamaduni
  - Uadilifu na kuheshimu utawala wa kisheria
  - Kuokuwepo kwa rushwa na maovu mengine
  - Jamii iliyoelimika na inayojiamini, inayojifunza kutokana na uzoefu wake na wa wengine na yenye kumiliki na kubaini agenda ya maendeleo yake

Siku ya Nane

- Makundi Mahsusi yanakutana kuunganisha rasimu ya mpango

Siku ya Tisa

- Halmashauri ya Kijiji kuweka vipaumbele vya malengo mahususi .
- Kuandaa Rasimu ya Mpango wa miaka mitatu.

Siku ya Kumi

- Kikao Maalum cha Kamati ya Maendeleo ya Kata kufanyika ili kutoa ushauri kwenye rasimu ya mipango ya miaka mitatu ya vijiji.

Siku ya kumi na moja

- Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji kupokea, kujadili na kupitisha mpango wa Kijiji

Siku ya Kumi na Mbili

- Kuunganisha mipango kisekta kwa kutumia fomu rahisi katika ngazi ya Kata